

**MKATABA WA UNUNUZI WA KOKOTO KWA AJILI YA
UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA HOSPITALI YA
RUFAA YA MKOA-IRINGA**

KATI YA

**MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA -
IRINGA**

NA

EXPANSE COMPANY LTD

MKATABA WA UNUNUZI WA KOKOTO KWA AJILI YA UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA-IRINGA

KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA-IRINGA

Sanduku la Posta 260 Iringa ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mwajiri kwa upande mmoja.

EXPENSE COMPANY LIMITED ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mzabuni kwa upande mwingine

KWA KUWA Mnunuzi anahitaji na yuko tayari kununua vifaa kwa ajili ya miundo mbinu ya mtandao vyenye thamani ya fedha shilingi **3,525,998.40** sawa na mchanganuo umeambatanishwa

HIVYO BASI pande zote mbili zinashuhudia makubaliano yafuatayo:

1. **KWAMBA** Mkataba huu niwamauziano ya kokoto kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi
2. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kuuza kokoto kulingana na mahitaji /orodha ya vifaa vilivyoorodheshwa katika nukuu ya bei iliyoambatanishwa katika mkataba huu
3. **KWAMBA** Bei iliyonukuliwa katika fomu ya nukuu ya bei iliyoambatanishwa haitabadilika katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.
4. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kutoa vifaa kulingana na orodha ya vifaa vilivyo katika fomu ya nukuu ya bei
5. **KWAMBA** Malipo yatafanywa baada ya vifaa kupokelewa na kukaguliwa kama ni timilifu na vinakidhi ubora unaotakiwa
6. **KWAMBA** Mkataba huu utafika kikomo baada ya vifaa kupokelewa na taratibu za malipo kukamilika

7. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kufanya kazi kwa uaminifu na pasipo kumsababishia hasara yoyote mwajiri.
8. **KWAMBA** Mnunuzi atakuwa na wajibu wa kuvunja mkataba muda wowote atakapona inafaa, pale atakapojiridhisha kuna ukiukwaji wa makubaliano katika mkataba
9. **KWAMBA** Endapo kutakuwa na hasara yoyote iliyosababishwa na muuzaji. Muuzaji atakuwa na wajibu wa kulipa gharama za hasara alizozisababisha au kukatwa malipo yake ilikufidia hasara iliyosababishwa
10. **KWAMBA** Endapo kama kutakuwa na ucheleweshwaji wa kazi uliosababishwa na muuzaji, mnunuzi atakuwa na wajibu wa kuvunja Mkataba
11. **KWAMBA** Mnunuzi atatoa kusudio la kuvunja Mkataba kwa maandishi ndani ya siku tatu
12. **KWAMBA** Mkataba huu ni halali kwa mujibu wa sheria za Tanzania na utatafsiriwa kwa mujibu wa sheria hizi.
13. **HIVYO BASI** Pande zote mbili zimeweka saina tarehe , mwezi na mwaka kama inavyoonyesha hapa chini:

Kwa ajili ya ushahidi wa makubaliano ya utekelezaji wa mkataba huu, pande mbili zinazohusika wameweka saina zao kama ifuatavyo:

YAMESAINIWA NA KUTOLEWA NA

Saini:.....

Jina: *Alfred M Laiso*



Cheo: **MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA- IRINGA (MNUNUZI)**

Tarehe:.....11/05/2022.....

Saini :.....

Jina: *HOBOKELA KAMAIULA*

Cheo: **SHAHIDI UPANDE WA MNUNUZI**

Tarehe.....11/5/2022.....